**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**

**SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

**Kumb . Na LSS/F. I - 2025** **Tarehe : 27/11/2025**

Jina la Mwanafunzi ------------------------------------------------------------------------

Shule ya Msingi ..........................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUGOBA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026**

**UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiuga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Lugoba.

Unatakiwa kufika shuleni bila kukosa tarehe 07/01/2025 siku ya Jumatano ufike kabla ya saa kumi jioni. **Usiporipoti nafasi yako tutawapa watoto wanaopenda kusoma LUGOBA SEKONDARI.** Kumbuka mmekaa kwa muda mrefu nyumbani tangu ulipomaliza elimu ya msingi.

**Kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya walete cheti cha kupimwa Afya kutoka hospitali ya serikali.**

Mkuu wa shule na wafanyakazi wote wa shule hii wanakupongeza na wanakutarajia uwe mwanafunzi **MTIIFU, NADHIFU, MWAMINIFU** na mshiriki wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI LUGOBA

.....................................................

ABDALLAH A SAKASA

MKUU WA SHULE



S.L.P 81, CHALINZE . Barabara ya Tanga , 61311 Lugoba Pwani.
Tovuti: www.lugoba.sc.tz , Simu ya Mkononi 0754 898 202
Email ya Mkuu wa Shule: alhajsakasa17@gmail.com

MAAGIZO NA MAHITAJI

Serikali imefuta michango yote isiyo na tija kwa shule za sekondari nchini kuanzia Novemba 27. 2015. Kufuatia Waraka huo namba 5 wazazi/walezi sasa wamebaki na majukumu yafuatayo-

- kumlipia kijana wake matibabu na nauli ya kwenda na kurudi shuleni kwa wale wanaotumia usafiri.
- Kwa mantiki hii mzazi/mlezi wa mtoto wa shule ya kutwa kama yetu hapaswi kulipa mchango wowote mwingine mbali ya matibabu; kama angekuwa anaishi nyumbani kwa wazazi au walezi wake.
- Lakini kwa kuwa shule yetu ina daharia (hostel) basi ni vema mzazi/mlezi ukisoma na kutekeleza maelekezo yafuatayo ambayo ni muhimu sana ili kufanya maisha ya vijana wetu wawapo shuleni kuwa mazuri hii ni kwa wanafunzi wote wa KUTWA
- **WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM HAWAHUSIKI NA MCHANGO WA CHAKULA WAKIWA SHULENI KWANI SERIKALI INAWAPATIA CHAKULA.**

SARE

WAVULANA:

1. Mpatie mwanao suruali mbili rangi nyeusi zishonwe marinda mawili mbele kila upande isiwe "Modal" (ya kubana).

2. Mpatie mwanao suruali mbili rangi ya "Dark Blue" zishonwe marinda mawili mbele kila upande isiwe "Modal" (ya kubana).

3. Mpatie mashati mawili (Tomato) rangi nyeupe mikono mifupi.

4. Mpatie Tshirt mbili nyeupe (shingo duara) zisizo na maandishi yoyote.

5. Viatu nyeusi vya ngozi vinavyofungwa kamba (Gidamu). Malapa na yeboyebo havitaruhusiwa kuingia navyo darasani kwani vitamfanya motto kuwa mnyonge na kutoshiriki vema katika tendo la kujifunza.

6. Shuka rangi ya kijana mbili au Zaidi.

7. Chandarua moja 3 x 6

8. Soksi nyeusi za kutosha.

9. Nguo za michezo Bukta na Tshirt rangi ya Blue.

10.Raba za michezo.

11.Nguo za ndani zisizopungua 6.

12.Aje na godoro upana futi 3 x unene inchi 4 na urefu kama kawaida futi 6.

**NB: Nguo za nyumbani na simu zinaweza kumfukuzisha mwanao shule.**

2

WASICHANA

1. Mpatie mwanao sketi mbili rangi ya kijani ndefu zinazopita magoti mshono wa V mbele (kama sketi za Polisi).

2. Mpatie mwanao sketi mbili rangi ya "Dark Blue" ndefu zinazopita magoti mshono wa V mbele (kama sketi za Polisi).

3. Mpatie mashati mawili (Tomato) rangi nyeupe mikono mifupi.

4. Mpatie Tshirt mbili nyeupe (shingo duara) zisizo na maandishi yoyote.

5. Viatu nyeusi vya ngozi vinavyofungwa kamba (Gidamu). Malapa na yeboyebo havitaruhusiwa kuingia navyo darasani kwani vitamfanya motto kuwa mnyonge na kutoshiriki vema katika tendo la kujifunza.

6. Shuka rangi ya "Light Blue" mbili.

7. Chandarua moja 3 x 6

8. Soksi nyeupe za kutosha.

9. Kanga au kitenge doti mbili.

10.Nguo za michezo Bukta na Tshirt rangi ya Blue (truck suit itafaa Zaidi).

11.Raba za michezo.

12.Aje na godoro upana futi 3 x unene inchi 4 na urefu kama kawaida futi 6.

13.Nguo za ndani zisizopungua 08.

14.Vihifadhio (Pad) Bunda nne au Zaidi.

**NB: Nguo za nyumbani na simu zinaweza kumfukuzisha mwanao shule.**

**WAISLAMU**

WASICHANA

Wanafunzi wasichana waislamu wanaruhusiwa kuvaa sketi ndefu , nusu kanzu kitambaa cha tetroni nzito siyo sukari na kijuba kinachofunika kifua cha kitambaa cheupe kama kilichoshona nusu kanzu.

**Kanzu kwa wavulana, kofia, kilemba na mapambo mengine haviruhusiwi shuleni**.

**GHARAMA ZA DAHARIA (HOSTEL) HII NI KWAAJILI YA WANAFUNZI WA KUTWA TU**

Shule ya sekondari Lugoba ni miongoni mwa shule za wananchi (Kata) za mwanzo sana. Shule hii ilianza mwaka 1989 ikiwa shule ya kutwa hivyo wanafunzi wake walikuwa wakipanga mitaani hapa katika mji wetu wa LUGOBA. Kwa bahati kubwa chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete** Rais mstaafu wakati huo akiwa Mbunge mwaka 2004 aliwezesha kujengwa kwa Daharia (hostel) ya wasichana, kupitia mhisani mkubwa wa shule hii N**dugu Subhash M M Patel.** Baada ya kuonekana wasichana kuishi vizuri katika mazingira mazuri **Mzee Subhash M M Patel** mwaka 2007 alijenga Daharia zingine kwaajili ya wasichana na kufanya ziwe tatu.

wanafunzi wetu wote kuishi shuleni. Hivyo wanafunzi wote wanaochaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Lugoba wanalazimika kuishi katika Daharia zetu. Ili maisha yaweze kuendelea akiwa hapa shuleni, mzazi/mlezi unapaswa kumlipia **jumla ya shilingi 140,000/=** ikiwa ni gharama za chakula kwa **muhula mmoja** sawa na **shilingi 280,000/= kwa mwaka**.. Kama serikali ilivyoelekeza kuwa wanafunzi wa shule za sekondari za kutwa kama hii, wazazi/walezi watawajibika kuwapatia watoto wao chakula, malazi, matibabu na nauli ya kwenda na kurudi shuleni. Hivyo ni vema sasa ukamlipia mwanao fedha hizo jumla ya **shilingi 140,000/= kwa muhula**. Tafadhali lipa fedha hizi kupitia akaunti namba **21101200009**

JINA LA AKAUNTI NI "**LUGOBA SEC. SCHOOL FUND**" iliyopo katika benki ya NMB tawi la Chalinze. **USIMLETE MTOTO BILA KUMLIPIA CHAKULA TAFADHALI SANA. LIPA FEDHA HIZO HARAKA KABLA YA JANUARI ILI TUJIANDAE KUMPOKEA MWANAO**.

**Mwanao atakula chakula utakacholipia wewe hakuna chakula kutoka kungine kokote usidanganywe.**

Aidha mpatie mwanao vifaa vifuatavyo kwaajili ya matumizi yake ya kibinaadam na kijamii:

1. Madaftari makubwa na peni za kutosha
2. Mkebe wa hesabu.
3. **Wavulana** wote waje na Jembe lenye mpini na **wasichana** wote waje na Panga kwaajili ya shughuli za usafi na kilimo
4. Fagio la chelewa lenye mpini.
5. Ndoo ndogo ya Lita 10 kwaajili ya matumizi yake.
6. Kamusi ya kiingereza.
7. Sahani, Kijiko na Kikombe visiwe vya Plastic.
8. Mswaki na dawa za meno za kutosha
9. Sabuni za kufuria na kuogea za kutosha.
10. Taulo moja au Zaidi.



S.L.P 81, CHALINZE . Barabara ya Tanga , 61311 Lugoba Pwani.
Tovuti: www.lugoba.sc.tz , Simu ya Mkononi 0754 898 202
Email ya Mkuu wa Shule: alhajsakasa17@gmail.com

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kupiga mwalimu au na mtu yeyote yule. 4

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na vywele fupi wakati wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(vii) Kufuga ndevu.

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumzi ya madawa ya kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi. (xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xiv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xv) Kudharau Bendera ya Taifa.

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kuywa sumu n.k.

(xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.



S.L.P 81, CHALINZE . Barabara ya Tanga , 61311 Lugoba Pwani.
Tovuti: www.lugoba.sc.tz , Simu ya Mkononi 0754 898 202
Email ya Mkuu wa Shule: alhajsakasa17@gmail.com

UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI LUGOBA

SEHEMU A (Ijazwe na Mwanafunzi).

Mimi (Jina Kamili ) ……………………………………………………… Nilizaliwa tarehe …………… Mwezi……………….. mwaka………………….. Dini ………………………..Katika Kijiji cha …………………. Wilaya ya …………............... mkoa wa .........................................

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha KWANZA Shule ya Sekondari Lugoba. Nathibitisha kuwa nitatii na kuzifuata sheria zote za Shule ambazo mwanafunzi analazimika kutekeleza na kutimiza ikiwa ni pamoja na kutokuwa na simu wala kuvaa nguo za nyumbani wakati wote nikiwa shuleni. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili uweze kutatua au kutafutia utatuzi wa changamoto zozote zitakazojitokeza Shuleni.

Saini -------------------------------------------------------

SEHEMU B: (Ijazwe na mzazi)

Mimi (Jina Kamili ) ………………………………………………………

Nilizaliwa tarehe ……………. Mwezi……………….. mwaka………………….. Dini ……………

Katika Kijiji cha ……………......wilaya ya .............…………. mkoa wa ..................... Kazi………………………… namba ya simu ya mzazi/mlezi...............................................

Nafurahi kupokea taarifa ya nafasi aliyopata mtoto wangu. Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitahakikisha mtoto anaenda Shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi …………………………………………

Jina la Mtendaji wa Kijiji ………………………………………….

Saini ya Mtendaji ……………………………………………….

MUHULI

*fomu hii iletwe siku ya kuripoti mwanafunzi ikiwa imejazwa kikamilifu



S.L.P 81, CHALINZE . Barabara ya Tanga , 61311 Lugoba Pwani.
Tovuti: www.lugoba.sc.tz , Simu ya Mkononi 0754 898 202
Email ya Mkuu wa Shule: alhajsakasa17@gmail.com